# JARIDA LA DODOJI

"Let's Us Share the Gift of Nature Together"

Januari -Juni, 2025 | Toleo Na. 03



**MPRU YASHIRIKI UZINDUZI WA MRADI WA KUTUNZA MSITU WA MLOLA WILAYA YA MAFIA**

...................... UK. 01

HALIUZWI

# YALIYOMO


01 MPRU YASHIRIKI UZINDUZI WA MRADI WA KUTUNZA MSITU WA MLOLA WILAYA YA MAFIA

02 WATAALAM KUTOKA BENKI YA DUNIA WATEMBELEA MAKAO MAKUU YA MPRU

03 MPRU YASHIRIKI SEMINA YA MAFUNZO YA 'SATELLITE REMOTE SENSING APPLICATION' NCHINI CHINA

04 MPRU YAFANYA KIKAO NA KAMATI YA USALAMA YA MKOA WA LINDI

05 WATUMISHI WATANO MPRU WATUNUKIWA VYETI MAFUNZO YA RESCUE DIVING, EMERGENCY FIRST RESPONSE

06 WATUMISHI MPRU WASHIRIKI MAADHIMISHO YA MEI MOSI 2025

07 MBREMP WATOA ELIMU YA UHIFADHI WA BAHARI NA MAZINGIRA KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI MSIMBATI

08 MPRU YAENDESHA PROGRAMU YA MAFUNZO KWA WANAFUNZI UDSM

09 WATUMISHI TACMP WAPATIWA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA MAKUSANYO YA NDANI 'MRPS'

10 NAIBU WAZIRI OMR-MUUNGANO NA MAZINGIRA ATEMBELEA BANDA LA MIFUGO NA MIFUGO NA TAASISI ZAKE

11 MKURUGENZI WA HALMASHAURI MTWARA ASHIRIKI ZOEZI LA USAFI NA KUPANDA MIKOKO MBREMP KATIKA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

12 MPRU YASHIRKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA UTALII YA KARIBU-KILI FAIR 2025

13 DKT. MPANGO ATAKA HATUA ZA PAMOJA NA MSHIKAMANO WA MATAIFA KATIKA UWEKEZAJI ENDELEVU WA BAHARI NA ULINZI WA BIOANUWAI

14 TACMP YASHIRIKI MAONESHO YA 12 YA BIASHARA NA UTALII TANGA

15 DKT. MAKAME ASISITIZA ZOEZI LA UTOAJI WA ELIMU KUHUSU UMUHIMU WA UTUNZWAJI WA MATUMBAWE

16 WARSHA YA KUBUNI MKAKATI WA USHIRIKIANO NA MAWASILIANO MAALUM MRADI WA CRRI

17 WAFANYAKAZI MIMP WAPATIWA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA KIDIJITALI WA TAARIFA ZA MIAMBA YA MATUMBAWE

18 PROGRAMU YA MAFUNZO MATUMIZI YA TEKNOLOJIA YA SMART MKOANI TANGA








**MARINE PARKS AND RESERVES TANZANIA (MPRU)**

S.L.P 7565, DAR ES SALAAM
+255 222150621
marineparks@marineparks.go.tz
www.marineparks.go.tz




# MPRU YASHIRIKI UZINDUZI WA MRADI WA KUTUNZA MSITU WA MLOLA WILAYA YA MAFIA

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki uzinduzi wa mradi wa kutunza msitu wa Mlola utakaoimarisha ustahimilivu wa mifumo ya Ikolojia ya misitu katika Kisiwa cha Mafia, uliofanyika tarehe 26 Mei, 2025.

Mradi huo uliozinduliwa na Shirika linalojihusisha na Uhifadhi wa Mazingira na Viumbe walio hatarini kutoweka Duniani (Sea Sense) unalenga katika kupambana na kudhibiti changamoto ya Mabadiliko ya Tabianchi ili yasilete madhara katika Msitu wa Mlola uliopo katika Kisiwa cha Mafia.

Akizindua mradi huo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Katibu Tarafa wa Kata ya Kusini Ndg. Taifa Constantine amelishukuru Shirika la Sea Sense kwa kushirikiana na Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia (MIMP), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), pamoja na Halmashauri kwa jitihada za kuanzisha mradi huo utakaosaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi. "Tumeshuhudia jinsi rasilimali zinavyomalizwa sehemu mbalimbali na zinavyoathirika na mabadiliko ya tabianchi, hivyo tunavyopata wadau kama hawa wanaokuja kurekebisha yaliyotokea, hatuna budi kuwapa ushirikiano ili kufanikisha adhma hiyo" ameeleza Ndg. Constantine.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Sea Sense, Ndg. Gosbert Katunzi ameeleza kuwa mradi huo ukitekelezwa vizuri na kuweka bayana changamoto na fursa zilizopo, utavutia wadau wengi ili waweze kuwekeza kisiwani Mafia.

Wadau mbalimbali wa mazingira wametoa wito kwa mashirika mengine kuunga mkono jitihada mbalimbali za utoaji wa elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira ili kuokoa rasilimali zilizopo.

"Tunashukuru shirika la Sea Sense kwa hatua mbalimbali wanazochukua kutunza mazingira, niwaombe mashirika mengine na wadau mbalimbali waunge mkono kutoa elimu kuhusu mazingira maana yanamgusa kila mtu na faida zake kila mtu anazijua, bila mazingira kila kitu kitatoweka" ameeleza Bw. Omari Abdallah, mkazi wa Mafia anayefanya kazi na Shirika la Sea Sense katika Uhifadhi wa Kasa.

Mradi wa kutunza msitu wa Mlola unatarajiwa kutekelezwa kwa miezi 18 katika Vijiji vitatu vya Kungwi, Kibada na Kifinge ambapo utaongeza ustahimilivu kwa jamii katika kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi.

# WATAALAM KUTOKA BENKI YA DUNIA WATEMBELEA MAKAO MAKUU YA MPRU



Na **Arafat Mnyau**

Wataalam kutoka Benki ya Dunia (World Bank) kupitia mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji wa Bahari Tanzania (TASFAM) wametembelea Makao Makuu ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) ili kujifunza na kujulishwa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na MPRU ikiwemo utekelezaji wa sheria na kanuni za Uhifadhi Bahari kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Tanzania Bara), Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (Zanzibar) na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imeandaa Mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji wa Bahari Tanzania kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Aidha, Tanzania hivi karibuni itaanza kutekeleza Mradi wa TASFAM (Tanzania Scaling up Sustainable Marine Fisheries and Aquaculture Management) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo kupitia ziara hiyo wataalamu hao kutoka Benki ya Dunia (World Bank) walipata fursa ya uelewa kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji wa sheria wa usimamizi wa rasilimali za bahari na kuthibiti uvuvi haramu.

Ziara hii inaashiria hatua muhimu katika kuimarisha ushirikiano kati ya serikali, wahisani, na wadau wa Uhifadhi wa mazingira ya Bahari kwa lengo la kufanikisha malengo ya endelevu.

Lengo ni kuhakikisha na kuona kuwa Mradi wa TASFAM unaboresha sekta ya uvuvi kwa kuwa na uvuvi endelevu na kulinda rasilimali za bahari.

Halikadhalika, mradi unalenga kuboresha upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa walengwana kuchochea kuongezeka kwa ajira kwa vijana wa Kitanzania. Mradi wa TASFAM unatarajiwa kutekelezwa katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi, ukihusisha Wilaya 17 za Tanzania Bara, Wilaya 11 za Zanzibar na ukanda maalum wa kiuchumi wa Bahari ya Hindi. Walengwa wa mradi huu ni jamii za mwambao zinazojihusisha na minyororo ya thamani ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji bahari.



# MPRU YASHIRIKI SEMINA YA MAFUNZO YA 'SATELLITE REMOTE SENSING APPLICATION' NCHINI CHINA

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki semina ya mafunzo ya ushirikiano kati ya China na Afrika kuhusu Matumizi ya Teknolojia ya Satelaiti kwa Ufuatiliaji wa Rasilimali (Satellite Remote Sensing Application), iliyofanyika kwa wiki mbili (2) kuanzia Februari 19 - Machi 04 2025 jijini Beijing, China.

Tanzania imewakilishwa na maafisa kutoka MPRU, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wizara ya Maliasili na Utalii, na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST), sambamba na wajumbe kutoka nchi nyingine saba (7) za Afrika pamoja na mwakilishi wa Umoja wa Afrika.

Mhifadhi Bahari, Bw. Mustapha Issa kutoka Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingiliano ya Mto Ruvuma (MBREMP) ameiwakilisha MPRU. Kupitia semina hiyo amepata ujuzi wa vitendo katika matumizi ya teknolojia ya remote sensing, ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa miamba ya Matumbawe, mabadiliko ya fukwe, na kubaini shughuli za uvuvi haramu.

Semina ilijikita katika matumizi ya teknolojia za kisasa za satelaiti, ikiwa ni pamoja na akili bandia (AI) na ujifunzaji wa mashine (machine learning), katika kusaidia ufuatiliaji wa mazingira, Uhifadhi wa bayoanuwai, na Usimamizi wa Rasilimali za Baharini.

Semina hiyo iliandaliwa na Kituo cha Ushirikiano wa China na Afrika kuhusu Matumizi ya Satelaiti (China-Africa Cooperation Center on Satellite Remote Sensing Application - CACSA), kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kiufundi na kubadilishana maarifa katika teknolojia ya satelaiti.

Mafunzo hayo yanatarajiwa kuimarisha uwezo wa MPRU katika shughuli za Uhifadhi wa rasilimali za bahari unaoongozwa na takwimu, pamoja na kusaidia maendeleo ya mifumo ya ufuatiliaji kwa muda halisi (real time) kwa ajili ya kuongeza ujuzi wa kiufundi na kuboresha juhudza Uhifadhi.



# MPRU YAFANYA KIKAO NA KAMATI YA USALAMA YA MKOA WA LINDI




Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imekutana na Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Lindi kujadili kikao kazi kuhusu Uhifadhi wa Visiwa vinavyopatikana katika Wilaya ya Kilwa.



Katika kikao hicho kilichofanyika Januari 09, 2025 katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, kiliongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, Mhe. Zainab Telack akiwa na Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Lindi na Wataalam kutoka MPRU akiongozwa na Mhifadhi Mkuu, Bw. Godfrey Ngupula.

Kikao hicho kilibeba dhima ya kuhifadhi visiwa vilivyopo katika Wilaya ya Kilwa ikiwemo Eneo Tengefu la Kilwa na kuilinda 'Gulf of Kilwa' na vivutio vyake ikiwemo Hifadhi ya Bahari ya Kilwa.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Zainab Telack alifurahia kusikia lengo la MPRU katika ikuhifadhi vivutio vilivyopo katika Wilaya hiyo na kuwataka wafanikishe kwa haraka zoezi hilo ikiwezekana kabla ya uzinduzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa uliyofikia zaidi ya 80% mpaka kukamilika kwake ambapo inatarajiwa kuzinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

# WATUMISHI WATANO MPRU WATUNUKIWA VYETI MAFUNZO YA 'RESCUE DIVING, EMERGENCY FIRST RESPONSE (EFR)



Na **Arafat Mnyau**

Watumishi watano (5) wa Hifadhi za Bahari na Maneneo Tengefu Tanzania (MPRU) wametunikiwa vyeti katika fani za 'Rescue Diving na Emergency First Response (EFR), kufuatia mafunzo ya wiki mbili yaliyofanyika katika Kisiwa cha Mafia.

Mafunzo hayo yaliwezeshwa na Shirika la Plongeurs Du Monde kutoka Ufaransa (Wapiga Mbizi wa Dunia) yenye dhamira ya MPRU katika kuimarisha uwezo wake wa kiutendaji pamoja na kulinda mazingira ya baharini ya Tanzania yenye thamani kubwa.

Watumishi wa MPRU waliokamilisha mafunzo haya kwa mafanikio ni Daniel Mallya, Hashim Kilawi, na Ailas Lema kutoka Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia (MIMP), Maria Pentzel kutoka Makao Makuu ya MPRU, pamoja na Kabodo kutoka Hifadhi ya Bahari ya Tanga Silikanti (TACMP).

Katika mafanikio ya kihistoria, Masanja Joram alishiriki mafunzo maalum ya kwanza kabisa duniani ya 'Eco-Guide Specialty' yenye ithibati ya PADI ambayo yatamwezesha kukuza utalii rafiki kwa mazingira na kuhakikisha mwingiliano endelevu na mfumo wa bahari.

Mpango huu wa kujenga uwezo ni hatua muhimu katika kuwawezesha watumishi wa MPRU kupata ujuzi wa msingi katika ufuatiliaji wa kina cha maji (underwater monitoring), mwitikio wa dharura (emergency response), na mwongozo wa utalii wa mazingira (eco-tourism guidance).

Mhifadhi Mfawidhi wa MIMP, Bw. Amin Abdallah pamoja na Mhifadhi, Mohamed Shamte walihudhuria hafla ya kutunuku vyeti na kuonesha fahari yao kwa mafanikio ya washiriki na kujitolea kwao katika kujifunza.

Plongeurs Du Monde pia wametia saini makubaliano (Memorandum Of Understanding) na mbuga za baharini za Tanzania kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wao wanaohusika na ulinzi wa viumbe vya baharini




# WATUMISHI MPRU WASHIRIKI MAADHIMISHO YA MEI MOSI 2025

Na **Arafat Mnyau**

Watumishi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) wameungana na wafanyakazi wengine duniani kushiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), ambayo kwa mwaka huu yameadhimishwa kitaifa katika Mkoa wa Singida, yakiongozwa na Mgeni Rasmi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Maadhimisho hayo yamebeba kauli mbiu isemayo "Uchaguzi Mkuu 2025 utuletee viongozi wanaojali haki na maslahi ya wafanyakazi, sote tushiriki," ikisisitiza umuhimu wa ushiriki wa wafanyakazi katika mchakato wa uchaguzi kwa ajili ya mustakabali bora wa haki zao.

Mhe. Rais Dkt. Samia akihutubia katika kilele cha sherehe hizo, ametangaza habari njema kwa wafanyakazi wote nchini kwa kutangaza ongezeko la kima cha chini cha mshahara kwa asilimia 35, hatua inayolenga kuboresha maisha ya mfanyakazi na kutambua mchango wao katika ujenzi wa taifa.

Maadhimisho ya Mei Mosi yameendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam, maadhimisho hayo yamefanyika kwa mafanikio makubwa yakiongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, Mhe. Albert Chalamila.









# MBREMP WATOA ELIMU YA UHIFADHI WA BAHARI NA MAZINGIRA KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI MSIMBATI

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi ya Bahari ya Ghuba Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma (MBREMP) kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii Mnazi Bay imetoa elimu kuhusu Uhifadhi wa Bahari na mazingira kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Msimbati iliyopo mkoani Mtwara.

Zoezi hilo la utoaji elimu ya kuwajengea uelewa wanafunzi hao iliongozwa na Ndg. Mwahija Alawi, Sospiter Wambura pamoja na Stellah Masai ambapo wanafunzi takribani 98 kutoka Shule ya Sekondari ya Msimbati waliweza kupatiwa elimu hiyo ya Uhifadhi wa Bahari na mazingira.

Moja ya jukumu kubwa kwa Idara ya Maendeleo ya Jamii Mnazi Bay kwenye Maeneo yaliyohifadhiwa ya Bahari (MPAs) ni kuhakikisha jamii inajengewa uelewa juu ya Uhifadhi wa Bahari na mazingira pamoja na kukuza juhudi za Uhifadhi shirikishi, matumizi endelevu ya Rasilimali za Bahari, kukuza fursa za Uchumiwa Bahari.








# MPRU YAENDESHA PROGRAMU YA MAFUNZO KWA WANAFUNZI UDSM

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tengefu Tanzania imeendesha programu ya mafunzo kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ili kuweza kufahamu na kujifunza shughuli mbalimbali zinazofanywa na MPRU.

Mafunzo hayo yaliyoanza kuanzia Februari 06 mpaka Februari 12, 2025 yakiongozwa na Afisa Masoko wa MPRU, Halima Tosiri akishirikiana na Afisa Uhusiano, Bw. Ivan Kimaro yalifanyika kwa mafaniko makubwa kwa kushuhudia idadi kubwa ya wanafunzi kutembelea Banda la MPRU lililopo katika viwanja vya chuo hicho kufahamu na kujifunza shughuli zinazofanywa na taasisi hiyo.




Wanafunzi hao walioweza kufika katika Banda la MPRU walipata fursa ya kujifunza kuhusiana na Utalii wa Bahari na shughuli za Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari zinavyoendeshwa ikiwa ni hatua moja wapo ya kuendana na sera ya Uchumi waBuluu kuhakikisha inakua kupitia rasilimali zetu za Bahari tulizonazo nchini.

Aidha, naye Afisa Utalii wa Dar es Salaam Marine R eserves System (DMRS), Bw. Sifuni Sospatery alishiriki kikamilifu katika programu hiyo ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi hao wa Chuo cha UDSM.



# WATUMISHI TACMP WAPATIWA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA MAKUSANYO YA NDANI 'MRPS'

Na **Arafat Mnyau**

Timu ya Wataalam kutoka Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imefanya zoezi la mafunzo ya mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato wa ndani ujulikanao kama 'Marine Reservation and Payment System' (MRPS) kwa watumishi wa kituo cha Hifadhi ya Bahari ya Tanga Silikanti (TACMP) kilichopo Mkoani Tanga.

Mafunzo hayo yaliongozwa na Afisa Tehama Bw. Yusuph Rajabu kuwajengea uwezo watumishi wa TACMP kuhusiana na mfumo na utendaji kazi wake ambapo mfumo huo mpya wa MRPS unatarajia kuchangiza weledi na umakini katika vituo vya makusanyo na kuchochea kuongezeka kwa mapato ya ndani.

Aidha, mafunzo hayo yalipatwa kuhudhuriwa na wadau wajulikanao kama 'Friend of Maziwe' ambao hujitolea kushiriki katika shughuli mbalimbali za Uhifadhi katika Kisiwa cha Maziwe.






# NAIBU WAZIRI OMR-MUUNGANO NA MAZINGIRA ATEMBELEA BANDA LA MIFUGO NA UVUVI NA TAASISI ZAKE

Na **Arafat Mnyau**

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. khamis Hamza Khamis ametembelea Banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Taasisi zilizopo chini yake kwa lengo la kufanya Ukaguzi kuhusu elimu inayotolewa na Wizara pamoja na Taasisi zake kwenye maonyesho Juni 04, 2025 katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Aidha, Taasisi zilizoshiriki kwenye maonyesho hayo ni pamoja na Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari kuu (DSFA), Bodi ya Nyama, Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO), Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) pamoja na Maabara ya Taifa ya Uvuvi.

Akizungumza katika Maonesho hayo, Mfahidhi Bahari kutoka



MPRU, Gister Nkini alisema wananchi wategemee kupata elimu ya utunzwaji wa mazingira ya Bahari pamoja na elimu ya kufanya urejeshaji wa Rasilimali za Bahari pamoja na urejeshaji wa taka za plastiki.

"Kazi zetu kubwa kwenye kuhifadhi bahari na kutunza mazingira ya bahari ni kufatilia rasilimali za bahari kama mikoko, matumbawe na nyasi bahari pia kufanya usafi wa fukwe zilizopo kuzikusanya, kuzichambua na kuzipelekea kwa wadau mbalimbali wanaofanya kazi za urejeshaji" alisema Gister Nkini.

Halikadhalika, aliongeza kuwa wao hufanya zoezi za urejeshwaji wa rasilimali za bahari zilizoharibika ikiwemo mikoko, matumbawe na nyasi bahari na kufanya doria kwaajili ya kutokomeza uvuvi haramu ambao sio endelevu katika maeneo ya Hifadhi.

# MKURUGENZI WA HALMASHAURI MTWARA ASHIRIKI ZOEZI LA USAFI NA KUPANDA MIKOKO MBREMP KATIKA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI




Na **Arafat Mnyau**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Ndg. Abeid A. Kafunda ameshiriki zoezi la usafi wa mazingira na kupanda mikoko katika fukwe za Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingiliano ya Mto Ruvuma (MBREMP) katika Kijiji cha Msimbati, Mkoani Mtwara.



Zoezi hilo la usafi na upandaji wa mikoko limefanyika June 05, 2025 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mkurugenzi wa Halmashauri wa Wilaya ya Mtwara ambaye alishirikiana na wadau kutoka M&P, Indian Ocean Conservation Alliance' (IOCA), wanafunzi pamoja na viongozi wa kijiji kutekeleza zoezi hilo.



MBREMP walishiriki zoezi hilo wakiongozwa na Mhifadhi Mfawidhi Dkt. Redfred Ngowo akiwa na wafanyakazi wengine ambapo kwa pamoja walishirikiana katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani yenye kauli mbiu isemayo "Mazingira Yetu na Tanzania ijayo Tuwajibike sasa; Dhibiti Matumizi ya Plastiki".




# MPRU YASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA UTALII YA 'KARIBU-KILI FAIR 2025'

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Utalii 'Karibu Kili Fair 2025' yaliyofanyika kuanzia Tarehe 06/06/2025 mpaka 08/06/2025 katika Viwanja vya Magereza, Mkoani Arusha.

Maonesho hayo yalifunguliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto na kueleza umuhimu wa jukwaa hilo katika kuwaunganisha watoa huduma, kutoa ajira na kunadi tamaduni zetu za asili kwa wageni washiriki.

"Kili-Fair 2025 si tu jukwaa la kutangaza vivutio vyetu, bali pia daraja la kuwaunganisha watoa huduma wa ndani na masoko ya kimataifa. Ni nafasi ya kuchochea ajira, mapato na thamani ya rasilimali zetu za kiutamaduni na kiasili"alisema Dr. Biteko.




Maonesho ya Kimataifa ya Utalii ya Karibu Kili-Fair ndiyo makubwa zaidi ya utalii Afrika Mashariki, ikihusisha washiriki zaidi ya 450 kutoka zaidi ya mataifa 30.

Ushiriki katika Tamasha hilo unaipa MPRU fursa ya kuweza kutoa elimu kwa wadau wake wote watakaotembelea katika Maonesho hayo juu ya shughuli za Uhifadhi wa Bahari na ulinzi wa rasilimali zake ikiwemo Matumbawe, Mikoko na Nyasi bahari.

Lengo kuu la tamasha hilo ni kukuza Utalii Tanzania na kuongeza ushirikiano wa kikanda baina ya Tanzania na Nchi za Afrika Mashariki.




# DKT. MPANGO ATAKA HATUA ZA PAMOJA NA MSHIKAMANO WA MATAIFA KATIKA UWEKEZAJI ENDELEVU WA BAHARI NA ULINZI WA BIOANUWAI

Na **Arafat Mnyau**

Makamu wa Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa Mataifa kuhakikisha kunakuwa na hatua za pamoja, mshikamano wa kimataifa, na uwekezaji endelevu ili kuhakikisha uchumi endelevu wa bahari, kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na kulinda bioanuwai ya baharini.

Makamu wa Rais ametoa wito huo wakati akihutubia Mkutano wa Tatu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Bahari (UNOC3) akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano huo unaofanyika Jijini Nice nchini Ufaransa.

Amesema hapana budi kuwa na hatua za ujasiri zikazoratibiwa kwa ufanisi ili kuhakikisha maendeleo makubwa katika uendelevu wa bahari.
Makamu wa Rais ameongeza kwamba ni muhimu kuongeza ufadhili katika kushughulikia changamoto za bahari, kwa kuzingatia zaidi kusaidia nchi za kipato cha chini na nchi zinazoendelea za Visiwa Vidogo, ambazo zinakabiliwa na ufinyu wa bajeti na mizigo ya madeni inayokwamisha kufikia ahadi zilizofanywa za utekelezaji wa Lengo la Maendeleo Endelevu namba 14.

Halikadhalika, Makamu wa Rais amesema ni muhimu kuhakikisha utekelezaji kamili wa Mkataba wa Bahari Kuu (BBNJ), kushughulikia tishio la uchimbaji madini wa bahari kuu usio endelevu pamoja na kuanzishwa kwa vyombo vya kisheria ili kukabiliana na uchafuzi wa plastiki.

Aidha, Makamu wa Rais amesema ni lazima kuwa na ushirikiano jumuishi na wenye usawa unaowezesha jamii za watu wa Pwani kuwa wahusika wakuu katika jukumu la kulinda na kuvumbua masuluhisho mbalimbali ya uendelevu wa bahari.






# TACMP YASHIRIKI MAONESHO YA 12 YA BIASHARA NA UTALII, TANGA

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga (TACMP) inashiriki ka tika Maonesho ya 12 ya Biashara na Utalii yanayofanyika katika Viwanja vya Mwahako katika Mkoa wa Tanga.

Maonesho hayo yalianza kuanzia Mei 28 hadi Juni 06, 2025, ambapo Mgeni Rasmi alikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dkt Batilda Burian.

Akizungumza katika ufunguzi rasmi wa Maonyesho ya 12 ya Biashara na Utalii yanayoendelea jijini Tanga, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dkt Batilda Burian amesema mkoa huo umejipanga kikamilifu kuweka mazingira bora ya uwekezaji.

Hotuba ya Mhe Balozi Dkt Batilda, imetolewa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mhe Dadi Kolimba, akisema mkoa una maeneo mengi yenye mvuto kwa uwekezaji, hususan katika sekta ya viwanda, na kwamba juhudi zinaendelea kuboresha miundombinu ya msingi ikiwemo barabara, maji, umeme na huduma za mawasiliano.

"Tunawahamasisha wafanyabiashara, wawekezaji pamoja na taasisi za umma na binafsi kutumia maonyesho haya kama jukwaa la kujifunza, kushirikiana na kutangaza bidhaa na huduma zao," alisema Dkt. Batilda.

Aidha, Afisa Utalii wa TACMP, Jamal Mvungi kwa kushirikiana na Afisa Utalii wa TMRS, Happiness Urio waliongoza ushiriki katika Maonesho hayo kwenye Banda kwa kunadi utalii wa Bahari, kuhamasisha kutembelea maeneo ya Uhifadhi na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na shughuli za Uhifadhi.

Serikali ya Mkoa imeahidi kuendelea kuimarisha mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na wawekezaji ili kukuza uchumi wa mkoa na tafa kwa ujumla. Maonesho hayo ya 12 ya Biashara na Utalii yalibeba Kauli Mbiu isemayo, "*Mwonekano wa Wadau Sekta ya Umma na Binafsi kwenye Uwekezaji, Ukuaji na Uendelevu wa Biashara*".

# DKT. MAKAME ASISITIZA ZOEZI LA UTOAJI WA ELIMU KUHUSU UMUHIMU WA UTUNZWAJI WA MATUMBAWE



Na **Arafat Mnyau**

Mkurugenzi wa Idara Uhifadhi wa Bahari kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Dkt. Makame Omar Makame amewataka Maofisa wa Uvuvi, Mameneja wa Hifadhi za Bahari pamoja na Wananchi kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuhifadhi Matumbawe baharini ili kuongeza uzalishaji wa samaki katika maeneo hayo.

Dr. Makame ameyasema hayo Skuki ya Tumekuja, Wilaya ya Mjini wakati alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja ya warsha ya utunzaji wa Matumbawe baharini.

Amesema matumbawe ya bahari yanapotumiwa vibaya na wavuvu samaki wanaozaliwa hupunguwa wakati wavuvi wanapofanya shuhuli zao hasa Uvuvi wa nyavu za kukokota hivyo aliwataka kutoa elimu lengo kuona kila mvuvi na mtumiaji wa Bahari anatunza matumbawe.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa Uhifadhi wa Matumbawe (CRRI) ambae pia ni Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) Bw. Gedfrey Ngupula amesema lengo la mkutano huo kwa makundi hayo ni kuona wavuvi wanakuwa na uelewa wa kulinda na Matumbawe kwa faida ya kizazi cha sasa na baadae.

Nao washiriki wa mkutano huo wamesema wamenufaika na mafunzo ya mkutano kwani wamepata uelewa wa kutuza matumbawe kwenye maeneo ya Hifadhi za Bahari.

Mkutano huo wa siku moja wa kuwajengea uwezo wasimamizi wa maeneo ya Baharini uliwashirikisha zaidi ya watu 100 na umelenga kutoa uelewa kwa jamii juu ya utunzaji wa Matumbawe baharini.





# WARSHA YA KUBUNI MKAKATI WA USHIRIKIANO NA MAWASILIANO MAALUM MRADI WA CRRI

Na **Arafat Mnyau**


Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) kupitia Mratibu wa Mradi wa Uokoaji wa Miamba Matumbawe (CRRI) na Mhifadhi Mkuu wa MPRU Bw. Godfrey Ngupula wamefungua warsha ya siku tatu (Mei 28-30, 2025) ya kubuni mkakati wa ushirikiano na mawasiliano maalum kwa ajili ya mradi wa Coral Reef Rescue Initiative National Hub nchini Tanzania.




Warsha hiyo inayofanyika katika Hoteli ya Peacock jijini Dar es Salaam, inaongozwa na Wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Queensland kutoka nchini Australia na kuwaleta pamoja wataalamu wa mawasiliano kutoka Tanzania na Madagascar kukuza ushirikiano wa Kimataifa na kubadilishana maarifa.

Malengo muhimu ya warsha hii ni pamoja na kuunda mkakati wa mawasiliano na ushirikiano maalum kwa CRRI National Hub, kutengeneza mpango wa utekelezaji unaoweza kufuatiliwa kwa ufanisi, kuimarisha uwezo wa washiriki katika kutekeleza na kuhamasisha mkakati huo kwa ufanisi.

Aidha, jitihada zinazofanywa na kufuatiliwa kwa ufanisi, ya mawasiliano ni moja ya hatua muhimu katika kulinda na kurejesha mifumo muhimu ya mazingira ya Miamba ya Matumbawe kwa vizazi vijavyo.



# WATUMISHI MIMP WAPATIWA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA KIDIJITALI WA TAARIFA ZA MIAMBA YA MATUMBAWE

Na **Arafat Mnyau**

Wafanyakazi wa Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia (MIMP) na Hifadhi ya Maeneo Hai (Biosphere Reserve) wamepatiwa mafunzo ya kujengewa uwezo kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa Kidijitali wa Kitaifa ujulikanao kama "Tanzania Coral Reef Database System".

Mafunzo hayo yaliyotolewa Juni, 05, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa MIMPBR na kuongozwa na Afisa TEHAMA, Bw. Abasi Maige yanalenga kuboresha ukusanyaji, Uhifadhi na uchakataji wa taarifa muhimu kuhusu Miamba ya Matumbawe na Bioanuai kwa ujumla wake, samaki na wanajamii nchini Tanzania.

Aidha, Matumizi ya mfumo huu mpya wa kidijitali unatarajia kuboresha utunzaji muhimu wa kumbukumbu wa taarifa, ufanisi na kuchochea uwajibikaji kwa wafanyakazi katika kutekeleza



shughuli za kulinda na kusimamia Rasilimali za Bahari katika Maeneo yaliyohifadhiwa ya Bahari (MPAs).



# PROGRAMU YA MAFUNZO MATUMIZI YA TEKNOLOJIA YA SMART, TANGA

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) yashiriki katika mafunzo ya kujengea uwezo kuhusu matumizi ya Teknolojia ya SMART (Spatial Monitoring and Reporting Tool), yaliyoandaliwa kwa lengo la kuimarisha mbinu za Usimamizi na Uhifadhi wa Bahari yaliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Nyinda Classic iliyopo Mkoani Tanga.

Mafunzo hayo ya siku tano (Mei 26-30, 2025) yanafadhiliwa na Shirika la Wildlife Conservation Society (WCS), ambalo linaendelea kushiriki kikamilifu katika kukuza uwezo wa Kitaasisi na kuimarisha usimamizi wa Rasilimali za Baharini kwa njia endelevu.

SMART ni programu ya kisasa yenye vifaa vya uchambuzi wa taarifa, iliyoundwa kusaidia juhudi za Uhifadhi kwa kuboresha ufuatiliaji wa Bayoanuwai, kuratibu doria kwa ufanisi zaidi, na kukabiliana na vitendo haramu kama vile uvuvi haramu.



Mafunzo haya yalilenga kuwajengea ujuzi watumishi wa MPRU katika ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa katika shughuli za doria, utayarishaji wa ripoti na ramani kwa ajili ya kusaidia maamuzi sahihi, ufuatiliaji wa viashiria vya utendaji, pamoja na kusawazisha mbinu za ukusanyaji wa taarifa katika maeneo tofauti ya Hifadhi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU TANZANIA

## Tembelea Tovuti Kufahamu Shughuli za Utalii katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu

"Let's Us Share the Gift of Nature Together"


**IMEANDALIWA NA**

ARAFAT MNYAU
(Mwandishi/Writer)

IVAN KIMARO
(Mhariri Mkuu/Chief Editer)

AILARS DAVID
HALIMA TOSIRI
(Wahariri Wasaidizi/Sub-Editors)

HELADIUS BAYINGANA
ABAS MAIGE
(Michoro & Usanifu/Graphics & Design)